Toleo 58 - Rabi ul Awwal 1443 AH / Novemba 2021 M

# UQAB
Jarida la

**TAARIFA KWA VYOMBO VYYA HARABI**
Mapenzi ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw) Yahitaji Kusimamishwa kwa Khilafah kwa Njia ya Utume

**HABARI NA MAONI**
Sera na Sheria za Kirasilimali za Kisekula Zinashambulia Kiungo cha Familia

**MATOLEO**
Je, Al-Aqsa Haina Salah ud- Din wa Kuitakasa kutokana na Najisi ya Mayahudi?

**JIBU LA SWALI**
Ubebaji wa Da'wah ni Faradhi ya lazima ama ni Faradhi ya Kutoshelezana?



Afisi ya Habari Wilayah Pakistan

بسم الله الرحمن الرحيم

﴿وَعَدَ ٱللَّهُ ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ مِنكُمۡ وَعَمِلُواْ ٱلصَّٰلِحَٰتِ لَيَسۡتَخۡلِفَنَّهُمۡ فِي ٱلۡأَرۡضِ كَمَا ٱسۡتَخۡلَفَ ٱلَّذِينَ مِن قَبۡلِهِمۡ وَلَيُمَكِّنَنَّ لَهُمۡ دِينَهُمُ ٱلَّذِي ٱرۡتَضَىٰ لَهُمۡ وَلَيُبَدِّلَنَّهُم مِّنۢ بَعۡدِ خَوۡفِهِمۡ أَمۡنٗاۚ يَعۡبُدُونَنِي لَا يُشۡرِكُونَ بِي شَيۡـٔٗاۚ وَمَن كَفَرَ بَعۡدَ ذَٰلِكَ فَأُوْلَٰٓئِكَ هُمُ ٱلۡفَٰسِقُونَ﴾

KUMB: 17/1443 Jumanne, 12 Rabi' I 1443 H 19/10/2021 M


Taarifa kwa Vyombo Vya Habari

# Mapenzi ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw) Yahitaji Kusimamishwa kwa Khilafah kwa Njia ya Utume

Mwezi wa Rabi ul-Awwal ni mwezi uliobarikiwa ambao Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw) alikuja hapa ulimwenguni. Ni wajibu kumpenda Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw), kumtanguliza (saw) kwanza juu ya kila jambo la kidunia, kwani ni wajibu kumtii (saw). Mwenyezi Mungu (swt) katika Surah At-Tauba, Ayah 24 amesema,

**[قُلْ إِن كَانَ آبَاؤُكُمْ وَأَبْنَآؤُكُمْ وَإِخْوَانُكُمْ وَأَزْوَاجُكُمْ وَعَشِيرَتُكُمْ وَأَمْوَالٌ اقْتَرَفْتُمُوهَا وَتِجَارَةٌ تَخْشَوْنَ كَسَادَهَا وَمَسَاكِنُ تَرْضَوْنَهَا أَحَبَّ إِلَيْكُم مِّنَ اللهِ وَرَسُولِهِ وَجِهَادٍ فِي سَبِيلِهِ فَتَرَبَّصُواْ حَتَّى يَأْتِيَ اللهُ بِأَمْرِهِ وَاللهُ لاَ يَهْدِي الْقَوْمَ الْفَاسِقِينَ]**

"**Sema: Ikiwa baba zenu, na wenenu, na ndugu zenu, na wake zenu, na jamaa zenu, na mali mliyo yachuma, na biashara mnazo ogopa kuharibika, na majumba mnayo yapenda, ni vipenzi zaidi kwenu kuliko Mwenyezi Mungu na Mtume wake na Jihadi katika Njia yake, basi ngojeni mpaka Mwenyezi Mungu alete amri yake. Na Mwenyezi Mungu hawaongoi watu wapotovu.**" Kwa hivyo, nini maana ya mapenzi kwa Mtume (saw)? An-Nawawi amesimulia maana ya mapenzi kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw) kutoka kwa Sulayman ibn al-Khattabi katika maelezo yake kuhusu Muslim, ambayo yanasema, "لا تصدُق في حبي حتى تفني في طاعتي نفسك، وتؤثر رضاي على هواك، وإن كان فيه هلاكك" "Huwezi kuwa mkweli katika mapenzi yangu isipokuwa ujitume kwa kunitii mimi na uweke radhi zangu mbele ya matamanio yako mwenyewe, hata ikiwa itakugharimu maisha yako." Kwa hivyo, mapenzi kwa Mtume (saw) leo hayawezi kuonyeshwa kupitia maneno matupu ya serikali ya 12 Rabii 'al-Awwal, mipangilio ya taa zinazong'ara ng'ara na domo tupu la likizo ya umma, bali kwa kupitia tu kusimamishwa kwa Khilafah kwa Njia ya Utume.

**Enyi Waislamu na Watu wao wanaomiliki Nguvu!** Leo Waislamu kote ulimwenguni wako katika rehema ya makafiri, katika hali ya umaskini na udhalilishaji kwa sababu ya mfumo wa Magharibi, huku watawala wao wakijifakhiri kuwa washirika wa maadui makruseda. Wakati heshima ya Mtume (saw) inachafuliwa kwa kuungwa mkono na dola za wakoloni wa Magharibi, watawala hawa wanakataa kumfukuza hata balozi mmoja, achilia mbali kuhamasisha vikosi vyetu vya majeshi ili mikono na ndimi ovu zikatwe. Hata baada ya kuona masaibu ya wale wanaompenda Mtume (saw) katika nchi za Waislamu zinazokaliwa kwa mabavu, watawala wetu wanawafunga minyororo vikosi vyetu kambini mwao. Kwa kuzingatia hali hizi zote, mapenzi wa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw) yahitaji kwamba nyinyi, kwa kumtii Nabii wenu kipenzi (saw), muwapindue watawala wasaliti wa sasa. Ni hapo tu ndipo mtakaporudisha nguvu ya umoja wa kisiasa, kupitia kurudisha Khilafah ambayo itairithi kikweli Dola ya Kiislamu aliyoianzisha Mtume (saw) mjini Al-Madina Al-Munawwarah. Hakika mapenzi ya Mtume wetu (saw) yanastahili zaidi kuliko mapenzi ya ulimwengu huu, watu wote waliomo ndani yake, biashara zetu na hadhi yetu. Lazima tushinde kila kikwazo na kuikumbatia kila hatari ili kumtii yeye (saw). Hili ndilo litakalotutumikia kikweli Siku ya Kiyama mbele ya Mwenyezi Mungu (swt), in shaa Allah na kutuleta karibu naye (saw) kesho Akhera. Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw) amesema, **«أَنْتَ مَعَ مَنْ أَحْبَبْتَ»** **"(Kesho Akhera) utakuwa pamoja na yule umpendae."** (Bukhari na Muslim).

**Afisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir**
**katika Wilayah Pakistan**



Email: info@uqab.or.ke

# Umuhimu wa Kutumia Mtandao wa Kibinafsi wa Kubuni (VPN) katika Zama za Uvamizi wa Tawala na Makampuni

Duniani kote wanadamu wanakabiliwa na ujasusi mpana, udhibiti na ufuatiliaji kutoka kwa tawala na makampuni. Ama tawala zinajaribu kulinda madaraka na uhalali wao dhidi ya kuhesabiwa kwao na watu kitaifa na kimataifa. Watu wanafichua kufeli kwa sera na sheria za tawala zilizojikita katika mfumo batili wa kirasilimali wa kisekula. Kwa upande mwingine, makampuni yanalenga kuzidisha mapato yao na kuwapiku washindani. Kila upande ima kwa kushirikiana au kila mmoja kivyake huweka mbinu na mipango ya kidijitali ili kuweza kushawishi upitishaji wa sera na sharia mpya au kuzikiuka zilizopo tayari ili kufikia malengo yao.

Natija yake ni kuwa idadi ya watu wanaojifunga na matumizi ya VPN inaendelea kuongezeka wakitafuta ulinzi dhidi ya hatari ya ujasusi, ukusanyaji wa taarifa zao na vitisho vya kiusalama. Kwa hiyo VPN inakuwezesha kuingia mtandaoni ukiwa na usalama na usiri zaidi. Kwa kuongezea, inakupa uwezo wa kuepuka udhibiti na kupata maudhui yaliyodhibitiwa. VPN ina uwezo wa kufanya yote hayo kwa kubuni kiunganishi kilicho na kodi baina ya kifaa/tarakilishi yako (desktop/ laptop/ tablet/ smartphone/ tv etc.) na sava ya VPN. Hivyo basi, unaingia mtandaoni kupitia kiunganishi kilicho na kodi na eneo lako ni kwa mujibu wa sava uliyojiunganisha nayo.

Ni muhimu kutambua kwamba unapoingia mtandaoni bila kutumia VPN kila unachofanya kinaweza kufuatiliwa hadi pale ulipo khaswa na kifaa unachotumia. Inawezekana kupitia anwani ya kifaa chako mtandaoni (IP). Inamaanisha kwamba unapotumia VPN eneo lako la kweli na anwani ya chombo chako hufichwa na badala yake kuchukua sava ya VPN unayotumia. Hata hivyo, wanaotoa huduma za mitandao (ISP) au yeyote anayefuatilia mtandao wako anaweza kuona kuwa umejiunganisha na sava ya VPN; lakini hawezi kurekodi taarifa zako (vitendo vyako mtandaoni). Pia, unapotumia VPN ni muhimu kutumia browser na kidhibiti matangazo imara. Daima ni bora kutumia VPN za kulipia na kuepuka za bure. Tafiti nyingi zinathibitisha kwamba VPN nyingi za bure zina rekodi, fichua na fanyia biashara taarifa za watumizi. Na VPN za kulipia zinakuwezesha kupangilia upya GPS yako na kuficha kuonekana kama umejiunganisha na sava ya VPN.

Kwa kufupisha VPN inatumika kwa sababu ya usiri, usalama na kuepuka udhibiti. Hususan VPN inakupa uwezo wa: 1- kutotambulika mtandaoni kwa kuficha anwani na eneo lako, 2- kuzuru tovuti na maudhui yaliyodhibitiwa, 3- ulinzi dhidi ya wadukuzi/majasusi unapotumia mitandao binafsi na ya ummah ya Wi-fi, 4- kulinda taarifa zako binafsi (neno la siri n.k).

Katika zama hizi ambapo mradi wa demokrasia unazama kutoka janga hadi janga, tawala zimeamua kutumia mbinu katili ili kuweza kuhifadhi mamlaka zao. Na katika kufanya hivyo wameweza kufichua uhadaifu ulipo wa kile kinachoitwa uhuru wa kibinafsi na uhuru wa maoni ambayo ni sehemu katika nguzo za demokrasia. Haishangazi kwani huko Amerika, wahudumu wa mitandao wanaweza kisheria kurekodi taarifa zako na kuziuza kwa watangazaji au kuzikabidhi vitengo vya ujasusi. Kwa kuongezea nchini Uingereza makampuni ya mitandao na simu yanatakiwa kisheria kurekodi taarifa zote za wateja wao (historia ya kubrowse, jumbe za simu na eneo walipo) na kisha kuzikabidhi vitengo vya Uingereza. Hilo linathibitisha mpango unaofuatwa na dola kuu ya zamani na ya sasa katika kiu chao cha kujilinda dhidi ya hasira za ummah kwa kuwatia hofu. Hali iliyoko kwa mataifa mengine ni ya kusikitisha!

Matumizi ya VPN yataendelea kuzidi kwani mizozo inaendelea kuzikumba serikali za kidemokrasia. Na kuwapelekea watu kutafuta njia na majukwaa mbadala ili kuweza kupaza sauti zao na kuwahesabu watawala wao.

Suluhisho la kimsingi ili kupatikane dunia salama inayotanua ikiwa ndani ya uhesabianaji na upataji taarifa za kweli unaweza kupatikana kupitia kusimamisha Dola ya Kiislamu ya Khilafah kwa njia ya Utume. Serikali ya Kiislamu ambayo haiwafanyii ujasusi raia wake isipokuwa pale itakapokuwa imeamrishwa na Shari'ah (Qur'an na Sunnah) kufanya hivyo tena katika dhurufu maalum kuhusiana na adui. Kwa kuongezea, itajizatiti kuwajenga raia wake kuwa na utambulisho wa Kiislamu. Hivyo basi raia wake watakuwa chini ya ushawishi wa utambulisho wa Kiislamu katika kuyaendea mambo yao ya kila siku.

Raia wanaoshawishiwa na utambulisho wa Kiislamu watajituma kuhakikisha kuwa kuna amani na utulivu ndani ya Khilafah. Kinyume chake yeyote atakayejihusisha na kuleta vurugu atahesabiwa kwa mujibu wa Shari'ah na wala sio kwa kutegemea hawaa za walioko madarakani kama inavyoshuhudiwa leo katika tawala hizi kandamizi duniani kote. Mtawala, Khalifah ni raia kama raia mwingine mbele ya Shari'ah na hana kinga kutokamana na vitendo vyake kama wanavyopewa watawala wa sasa (marais/wafalme/mawaziri wakuu n.k). Khilafah itachora na kutekeleza sera pana itakayowaelekeza raia namna ya kutumia mtandao na huduma zinazaohusiana na teknolojia. InshaAllah.

**Ali Nassoro Ali**
**Mwanachama wa Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir**

# HABARI NA MAONI ▪ Sera na Sheria za Kirasilimali za Kisekula Zinashambulia Kiungo cha Familia

**Habari:**

Vyombo vya habari nchini Kenya vimeripoti kwamba Hakimu wa Mahakama Kuu, Teresia Matheka ametangaza kwamba kuwa mke nyumbani lazima izingatiwe kuwa ni kazi kamili yenye kustahili malipo. Hakimu alisema: “Ni rahisi kwa mwanandoa anayefanyakazi mbali na nyumbani na kutumana pesa kudai mali yote iliyonunuliwa na kuendelezwa kwa kutumia pesa alizotuma na mwanandoa anayekaa nyumbani na kuwasimamia watoto na familia. Mwanandoa huyo atasikika akisema kwamba yule mwingine hakuwa ameajiriwa na hakutoa mchango wowote.  Kuwalea watoto ni kazi kamili ambayo familia humlipa mtu kufanya pamoja na kupika na kusafisha. Hivyo basi, kwa mwanamke aliyeajiriwa ambaye hulazimika kuwajibikia kubeba mimba na kuilea lazima mchango huu uzingatiwe.”

**Maoni:**

Matangazo hayo ni natija ya fursa iliyopatikana kwa kujifunga na mfumo wa kirasilimali wa kisekula na nidhamu zake ovu. Ni muhimu kutambua kwamba punde wanadamu wanapokwenda kinyume na njia ya Muumba wao -Mwenyezi Mungu (swt), basi hawaa na matamanio ndiyo yanayowaongoza na kuingia katika maangamivu. Hakika, sera na sheria za kirasilimali za kisekula kama vile Kifungu 45(3) cha Katiba ambacho kimetia ndani ya sheria ya Kenya malengo ya Mkataba wa Kumaliza Ukandamizaji Dhidi ya Wanawake ili kupatikane usawa ndani ya ndoa kwa kuwezesha ‘pande zote katika ndoa kupata haki sawa wakati wa kufunga ndoa, kipindi cha ndoa na kuvunjika kwa ndoa.’ (The Star, 10/10/2021).

Sera na sheria hizo zinachipuza kutoka katika akili finyu za wanadamu ambao wamechukua dori ya kujitungia sheria wenyewe badala ya kujisalimisha kwa maamrisho na makatazo ya Muumba wao. Kwa kuongezea, sera na sheria hizo hupelekea kuchochea chuki zaidi na ushindani duni ndani ya kiungo cha familia ambacho tayari kimesambaratika kwa kuwa misingi yake yenye nyufa imetokamana na nidhamu ya kijamii huria. Nidhamu hatari ya kijamii ambayo inapigia debe aina zote za mahusiano mfano yale yanayoitwa mahusiano ya wazi ambapo mume au mke anaweza kuwa ndani ya ndoa lakini anashiriki vitendo vya ngono na watu wengine! Nidhamu ovu ya kijamii ambayo inawatizama wanachama wa jamii kwa sura ya uzalishaji wa kiuchumi pekee! Hivyo basi, kuifanya taasisi ya ndoa kuwa ni sehemu ya ushindani wa kiuchumi baina ya waliooana.

Sera na sheria za kirasilimali za kisekula zimehalalisha LGBTQ na kuwapa uwezo wa kutafuta ulinzi wa kisheria pale ambapo ‘haki zao’ zinapokiukwa. Takwimu za hivi karibuni zinaashiria kwamba idadi ya LGBTQ inazidi ilhali idadi ya wanaoana inapungua huku viwango vya talaka vikizidi duniani kote. Hatimaye, sera na sheria hizi zipo kwa ajili ya kuzidisha sintofahamu kwa wanachama waliobakia ndani ya taasisi ya ndoa. Kwani mizozo kwa ajili ya mali miongoni mwa wanandoa itaendelea na kuzidi kwa sababu nia msingi ya kuingia katika ndoa ni kwa ajili ya ustawi wa kiuchumi kwa gharama yoyote ile kwa mfano kuwatumia watoto kama ndoano ya kifedha! Na kuwapelekea wanandoa kuwa ni zana za ngono!

Kwa upande mwingine, mfumo wa Kiislamu unaochipuza kutoka kwa Muumba wa ulimwengu, mwanadamu na uhai –Mwenyezi Mungu (swt); unaamrisha ndoa kuwa ni kitendo cha ibada. Kwa hivyo, kama vilivyo vitendo vyote vya ibada lazima vifuatiliwe kwa nia safi ambayo ni kukuza familia makini ambayo itapelekea kuwepo kizazi ambacho kitamuogopa Mwenyezi Mungu (swt) kwa kujifunga na kipimo cha Halali na Haramu katika kupima vitendo vya wanadamu. Katika Uislamu, ndoa ni sehemu ambapo mume na mke/wake hupata faraja, utulivu na upendo. Kwa kuwa ndoa ni fungamano la hiyari baina ya mume (Muislamu) na mke/wake; na hakuna anayelazimishwa juu ya mwingine. Kwa mujibu wa Shari’ah wote mwanamume na mwanamke wako sawa ima wamo katika ndoa au la. Vilevile, Shari’ah imepambanua dori maalumu ambazo kila mmoja anatakiwa kujifunga nazo ndani ya mujtama jumla na katika ngazi ya familia.

Kwa kutamatisha, ripoti nyingi zinazopeperushwa na vyombo vya habari kama vile kuzidi kwa viwango vya talaka, watoto wa mitaani, familia zilizovunjika, kujitoa uhai na mauji katika ndoa n.k. Yote hayo ni sehemu ya kufeli kwa sera na sheria za kirasilimali za kisekula ambazo zinachipuza kutoka katika akili zenye kikomo za wanadamu. Kwa hivyo, vyombo vya habari vilitakiwa viwe vinaangazia chanzo cha majanga haya ya kijamii yasiyohesabika yanayokumba ulimwengu. Badala ya kupeperusha sehemu baadhi ya hukumu ya Mahakama Kuu inayodai kuwalinda washirika katika ndoa kutokamana na ukandamizaji wa kiuchumi. Kwani, ndoa kwa mujibu wa nidhamu ya kijamii huria ni ushirika baina ya watu wazima walioridhiana! Ni chini ya nidhamu ya kijamii ya Kiislamu ndipo wanandoa watakapo shuhudia amani na utulivu. Mwenyezi Mungu (swt) asema

وَمِنْ آيَاتِهِ أَنْ خَلَقَ لَكُم مِّنْ أَنفُسِكُمْ أَزْوَاجًا لِّتَسْكُنُوا إِلَيْهَا وَجَعَلَ بَيْنَكُم مَّوَدَّةً وَرَحْمَةً إِنَّ فِي ذَٰلِكَ لَآيَاتٍ لِّقَوْمٍ يَتَفَكَّرُونَ **“Na katika ishara zake ni kuwa amekuumbieni wake zenu kutokamana na nafsi zenu ili mpate utulivu kwao. Naye amejaalia mapenzi na huruma baina yenu. Hakika katika haya bila shaka zipo ishara kwa watu wanao fikiri.” [30. Ar-Rum: 21].**

**Ali Nassoro Ali**

**Mwanachama wa Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir**

# Alama za Mapenzi ya MwenyeziMungu Kwa Mja Wake

Mara nyingi,mahaba huarifishwa kuwa hisia zenye mvuto mkubwa na muambatanisho wa kimwehemko. Watu wengi hufunga maana ya mapenzi katika muktadha wa vitu na anasa na starehe za duniani. Kwa kuwa ni mapenzi ni mchakato wa maumbile ya mwanadamu, hivyo siajabu kuyaona mapenzi na upendo yamekita katika jamii ya kibinadamu. Mapenzi ya mume kwa mkewe, Baba kwa wanawe na mapenzi ya mtu ya sehemu anayoishi yote hii ni mifano tu michache inayothibitisha uwepo wa tunu hii kubwa ulimwenguni. MwenyeziMungu SWT alimuumbia mwanadamu sifa ya kupenda sana mali kama alivyobainisha katika suratul Aadiyat:

وَإِنَّهُ لِحُبِّ ٱلْخَيْرِ لَشَدِيدٌ

**Kwa hakika kupenda kwake mali kukubwa mno.**

Tafsiri hii ya mapenzi ni katika mafungamano baina ya waja. Ama kuhusu sifa ya MwenyeziMungu kupenda waja wake hii humaanisha kumtunukia mja neema ya msamaha. Na ni ukubwa gani huu ulioje wa neema hii ya kupendwa na Mwenyezi Mungu Muumba Mbingu na Ardhi na vilivyomo? Quran imethibitisha kuwa MwenyeziMungu huwapenda waja wake wema kama alivyosema katika suratul Maidah aya 54:

فَسَوْفَ يَأْتِي ٱللَّهُ بِقَوْمٍ يُحِبُّهُمْ وَيُحِبُّونَهُ

**Basi MwenyeziMungu atawaleta watu ambao atawapenda nao watampenda.**

Kabla ya kuweka hapa alama zinazoashiria kuwa mja anapendwa na MwenyeziMungu, ni muhimu sana kuzindusha kuwa mapenzi ya MwenyeziMungu kwa waja wake yamefungamanika na kujifunga na taklifu za kisheria yaani wakati wowote mja anapojifunga na maamrisho ya MwenyeziMung na kujiepusha na makatazo yake. Hii ndio kujiwekea dhamana nzuri ya kuyapapata mapenzi ya Allah. Hii ndio sababu ya Mtume (SAAW) katika kuomba kwake mahaba ya Mola wake, alikuwa akiomba amali itakayomfikisha kwenye mahaba hayo. Amepokea Tirmidhy kutoka Abi Dardai kwamba Mtume Rehma na Amani za MwenyeziMungu zimshukie Yeye alisema

«..كَانَ مِنْ دُعاءِ دَاوُدَ: اللَّهُمَّ إِنِّي أَسْأَلُكَ حُبَّكَ، وَحُبَّ مَنْ يُحِبُّكَ، وَالعَمَلَ الَّذِي يُبَلِّغُنِي حُبَّكَ، ».

Katika dua za Daud AS : **Ewe Mola nakuomba mahaba yako na Mahama ya yule unayempenda na amali itakayonikisha kwenye mahaba yako..**

**Kwanza:Kupendwa na watu hapa duniani.**

Ukijiona kuwa waja wema wanakutaja kwa uzuri na hufurahi kila unapokutana nao basi ni ishara kuwa MwenyeziMung anakupenda. Abu Hureira anasimulia Hadithi kutoka kwa Mtume

إنَّ اللهَ تعالى إذا أحب عبدًا دعا جبريل، فقال: إني أحب فلانا فَأَحْبِبْهُ، فيحبه جبريل، ثم ينادي في السماء، فيقول: إن الله يحب فلاناً فأحبوه، فيحبه أهل السماء، ثم يوضع له القَبُولُ في الأرضِ،

MwenyeziMungu pindi anapompenda mja, humuitwa Jibril na kumwambia: Hakika yangu mimi ninampenda fulani nawe mpende na hapo jibril humpenda mtu huyu. Kisha Jibril hutangaza kwa Malaika wenzake mbinguni akisema: MwenyeziMungu anampenda fulani basi nanyi mpendeni. Hapo viumbe hao watukufu humpenda kisha huwekewa Qabul kwa hapa duniani.(Watu wakawa wanampenda.)

**Pili: Kuipa nyongo/Mgongo Dunia**

Hii ni moja wapo ya alama za kujulisha mtu kuwa ametunikiwa mapenzi ya Allah. Mmoja katika wanavyuoni mkubwa Sufyan Thauri alisema kwamba Zuhd hapa duniani ni kumaanisha kuwa uko tayari moyoni mwako kwa kufikiria Akhera kuwa kivyovyote vile utakufa.' Hivyo Kuipa nyongo dunia ni hali ya moyo wa mtu zaidi kuwa kwamba hotoishi milele hapa duniani bali ataihama. Tukiwa na ufahamu huu tutakua na hisia ya kwamba tutaondoka hapa dunia hii itatupelekea kutofitinika na starehe za dunia na tutajikurubisha zaidi kwa MwenyeziMungu kwa kujifunga na maamrisho yake na kuepuka makatazo yake. Hii humaanisha kutofitinika kabisa na mali, watoto na wanawake. Leo ulimwengu yanarembeshwa na mfumo wa kirasilimali ambao kila uchao utaona unavumbua fitina mpya za kumfanya mtu aone kuwa dunia ndio kila kitu. Runinga majumbani mwetu zimesheheni ya ulevi 'kata kiu na Tusker' yanayohadaa watu wengi kuamini kuwa maisha ya duniani ndio kila kitu hivyo watu ni kufukuza tamaa za mali! kujenga ufahamu kwamba ufanisi hapa duniani upo katika kufikia upeo mkubwa wa kukimu mahitaji yako ya kimwili hivyo fanya utakalo pasina na kujali halali au Haramu! Hali hii ndio hufanya watu wamecharukwa katika kutafuta 'maisha bora' huku wakiona kuwa hawana wakati kabisa kuutumikia Uislamu. Alikuja mtu mmoja kwa Mtume Rehema na Amani za MwenyeziMungu zimshukie akimuuliza

***Endelea... UK 6***



Email: info@uqab.or.ke

**Nijulishe ewe Mjumbe wa MwenyeziMungu amali nitakayoifanya itanipelekea kupendwa na MwenyeziMungu na kupendwa na watu. Mtume SAAW akwambia ni Ipe nyongo dunia Allah atakupenda  na achana kutamani vitu vya watu watakupenda watu.**

**Tatu: Upole na waja wenzako**

Hakuna tabia inayovutia watu wengi kama kuwa na upole katika kila jambo tena mahala panapostahiki. Upole hapa ni kuwa na busara iliojaa hekima katika kila jambo. Kwa mfano kumwambia Muislamu anayafahamu kwamba njia ya kusimamishwa kwa dola ya Kiislamu ni kupitia kujenga imani …Mwambie ndugu yangu kuna tofauti baina ya kulingania mtu imani na kulingania kurudisha maisha ya Kiislamu. Hii tofauti lau utambwambia wewe ni zuzu ! Kinyume chake ni busara kumwambia ewe ndugu yangu umejua jambo moja lakini umepitwa na mambo mengi kisha uanze kumwelezea njia halisi ya kisheria ya kusimamisha Darul Islam. Hivyo hivyo tunapotangamana na wake zetu majumbani tunatakikana kujipamba na sifa ya upole. Si hekima kabisa kumtukana  mkeo kwa sababu tu amevunja kikombe!

**Nne: Subra**

MwenyeziMungu SWT amakariri katika Quran sifa ya subra kwamba yeye siku zote yuko pamoja na wenye kusubiri. Sifa hii ni muhimu sana katika maisha ya Mwislamu. Ni katika suna ya MwenyeziMungu kuwatahini waja wake kwa maradhi, njaa, ukame vifo na kadhalika. Isitoshe subra inahitajika zaidi leo hususan tukizingatia kuwa kazi kubwa ilioko mbele yetu ni kuregesha tena Khilafah, bila shaka njia yake ni yenye kusuhubiwa na mazito. Uvumi dhidi ya Ujumbe unaobebwa, mateso ya walinganiaji na mengineo ni katika masaibu yanayokumba njiya ya mabadiliko. Asema Allah katika aya 146 ya suratul Imran:

وَكَأَيِّن مِّن نَّبِيٍّ قَاتَلَ مَعَهُ رِبِّيُّونَ كَثِيرٌ فَمَا وَهَنُواْ لِمَا أَصَابَهُمْ فِي سَبِيلِ اللهِ وَمَا ضَعُفُواْ وَمَا اسْتَكَانُواْ وَاللهُ يُحِبُّ الصَّابِرِين

Na manabii wangapi walipigana na maadui na pamoja nao kulikuwa na watakatifu wengi na hawakulegea kwa yale yaliyowasibu katika njia ya Mwenyezi Mungu, hawakudhoofika wala kudhalilika. Na MwenyeziMungu anawapenda wenye kusubiri.

Mwenyezimungu kutangaza kuwa anapenda wenye kusubiri ni amri kwa Waislamu kujipamba na subra kama vilevile subra ni alama ya kunali mahaba ya Allah.

**Tano: Kumfuata Mtume katika yote aliyotuamrisha na Kutukataza:**

MwenyeziMungu anasema:

قُلْ إِنْ كُنْتُمْ تُحِبُّونَ اللَّهَ فَاتَّبِعُونِي يُحْبِبْكُمُ اللَّهُ وَيَغْفِرْ لَكُمْ ذُنُوبَكُمْ ۗ وَاللَّهُ غَفُورٌ رَحِيمٌ

Kitendo hiki moja kwa moja hutupelekea kupata mahaba ya MwenyeziMungu SWT. Katika safu ya Waislamu kuna ulinganizi unaokaririwa sana wa kufuata sunna za Mtume SAAW. Na hili ni jambo zuri ispokuwa kufuatwa Mtume SAWW kumedogoshwa mno leo kiasi cha kuwaona Waislamu wanamfuata katika kuta nne na misikiti huku maisha jumla wakimuasi Mtume SAAW wakifuatwa siasa za  Biden na Boriss Johnson. Waislamu hawafuati uchumi wa Mtume Muhammad SAAW badali yake ni wafuasi wa mfumo wa Kirasilimali uliotungwa Adam Smith. Hawafuati tabia za Mtume SAAW bali wanafuata mienendo ya kileberali za kina John Lokce! Kama kweli unaona kuwa unamfuata Mtume SAAW katika kila jambo lako basi ni alama nzuri kuwa Allah anakupenda.

Hizi ni alama tano lau Muislamu ataonekana kuwa nazo basi ni dalili nzuri ya kuwa amenali mahaba ya ALLAH. Kwa hakika Mahaba ya Allah ni kitu cha thamani kwa mja kukikimbilia. Bahati nzuri ilioje Mtume SAAW akabainisha njia ya kuyafikia mahaba haya kama ilivyokuja katika hadith Qudusi

وما تقرب إليّ عبدي بشيء أحب إليّ مما افترضته عليه ، ولا يزال عبدي يتقرب إليّ بالنوافل حتى أحبه ، فإذا أحببته كنت سمعه الذي يسمع به ، وبصره الذي يبصر فيه ، ويده التي يبطش بها ورجله التي يمشي بها ، ولئن سألني لأعطينه ، ولئن استعاذني لأعيذنه

Na hajikurubishi kwangu mja wangu kwa jambo ninalolipenda zaidi ila kwa mambo ya faradhi niliyomfaradhishia. Na wala hatoacha mja kujikurubisha kwangu na suna bali akiendelea na ibada za sunna hufikia mimi Kumpenda. Na nitakapompenda, basi ninakua masikio yake anayosikia kwayo. Na Macho yake ambayo kwayo huonea na mkono wake ambao kwake hushikia na mguu wake anaoutembelea na endapo akiniomba humpa na akiniomba ulinzi mimi humlinda.

Na twamuomba MwenyeziMungu atupe mapenzi yake.

**Shabani Mwalimu**
**Mwakilishi kwa Vyombo Vya Habari, Hizb ut Tahrir Kenya**

# Je, Al-Aqsa Haina Salah ud- Din wa Kuitakasa kutokana na Najisi ya Mayahudi?

Sifa njema zote ni kwa Mwenyezi Mungu, Al-Qawi Al- Aziz, sifa njema zote ni kwa mwenye kuwanusuru waumini, sifa njema zote ni kwa yule asemaye:

سُبْحَانَ الَّذِي أَسْرَى بِعَبْدِهِ لَيْلاً مِنَ الْمَسْجِدِ الْحَرَامِ إِلَى الْمَسْجِدِ الْأَقْصَى الَّذِي بَارَكْنَا حَوْلَهُ لِنُرِيَهُ مِنْ آيَاتِنَا إِنَّهُ هُوَ السَّمِيعُ الْبَصِيرُ

**“SUBHANA, Ametakasika aliye mchukua mja wake usiku mmoja kutoka Msikiti Mtukufu mpaka Msikiti wa Mbali, ambao tumevibariki vilivyo uzunguka, ili tumuonyeshe baadhi ya Ishara zetu. Hakika Yeye ni Mwenye kusikia na Mwenye kuona”** [Al-Isra: 1] Rehma na amani nimshukie Mtume wa uongofu aliyesema:

وَلَيُوشِكَنَّ أَنْ لَا يَكُونَ لِلرَّجُلِ مِثْلُ شَطَنِ فَرَسِهِ مِنَ الْأَرْضِ حَيْثُ يَرَى مِنْهُ بَيْتَ الْمَقْدِسِ خَيْرٌ لَهُ مِنَ الدُّنْيَا جَمِيعاً

**“Na ni hakika kwamba zinakuja zama ambapo, mtu kuwa na ardhi mithili ya kamba ya farasi wake ambamo ataiweza kuiona Bai al-Maqdis ni bora kuliko dunia!”**

**Enyi mjumuiko uliobarikiwa, Enyi Waislamu mlioko kila mahali:**

Katika kumbukumbu ya maadhimisho ya ukombozi wa Jerusalem kutokana na karaha ya Makruseda, umbile la Kiyahudi linaidhinisha sheria inayofungua wazi mlango wa kuugeuza Msikiti wa Al-Aqsa kuwa sinagogi la Kiyahudi ambamo watafanya ibada na sala zao. Na wadhalilifu hawa katika viumbe wa Mwenyezi Mungu hawangeweza kufanya uhalifu huu na kukichafua Qiblah cha kwanza cha Waislamu lau si kwa khiyana ya wasaliti na njama ya watawala wahalifu. Hivyo basi, je! Mtaiacha Masra (eneo la Isra) ya Nabii wenu itekwe nyara na adui yenu?

**Enyi Waislamu:** Msikiti wa Al-Aqsa unakabiliwa na jaribio kubwa na shambulizi kali na ovu la umbile la Kiyahudi kulazimisha matambiko yao ya kibiblia katika Msikiti wa Al-Aqsa kwa maandalizi ya kuanzishwa kwa lile linalodaiwa kuwa hekalu lao katika eneo zima la Msikiti wa Al-Aqsa, kama ilivyoripotiwa na Wakfu wa Kimataifa wa Al-Quds katika ripoti yake ya hivi karibuni.

Tangazo la mahakama za umbile la Kiyahudi la haki ya walowezi ya kutekeleza maombi yao katika Msikiti wa Al-Aqsa ni **tamko la vita dhidi yenu**, na ni hatua hatari ya kuchukua udhibiti wa Msikiti wa Al-Aqsa.
Ni sawa na kile walichokifanya Makruseda baada ya kuikalia mnamo 1099 waliposimamisha msalaba wa dhahabu kwenye Kuba Al-Sakhra na kuigeuza kuwa kanisa. Walifanya vivyo hivyo kwa Msikiti wa Al-Qibli na kuuchafua Msikiti wa Al-Aqsa na majengo yake; baadhi yao yalibadilishwa kuwa mazizi ya farasi. **Je! Ni hatua gani mtakazochukua, enyi Waislamu?!**

Kilichowapa ujasiri umbile oga la Kiyahudi kuchukua hatua hii ni kwamba imepata watawala wasaliti, wenye kusalimu amri na wasawazishaji mahusiano! Watawala wa Falme za Kiarabu wanapokea viongozi wake, watawala wa Bahrain wanapeleka misheni na ndege, watawala wa Sudan na Morocco wanatia saini makubaliano nalo, Farauni wa Misri anafanya kila linalowezekana kuunda mazingira ya amani ambayo yatawawezesha kujitolea kwa ajili ya Ukingo wa Magharibi na Msikiti wa Al-Aqsa, na Mfalme wa Jordan analinda upande wao wa mashariki.

Msikiti wa Al-Aqsa sio bidhaa ya mazungumzo, wala mahali pa kushirikiana, na sio mahali pa kushindania juu ya udhamini rasmi. Msikiti wa Al-Aqsa ni mahali pa swala ya Manabii, mahali pa Mi'raj (kupaa mbinguni) kwa Nabii wenu Muhammad (saw), na Qibla chenu ambacho mlikuwa mkiswali mkikielekea mwanzoni mwa Uislamu. Na ni msikiti wa tatu ambao Waislamu wanaweza kusafiri kuuendea. Je! Al-Aqsa inapaswa kuachwa, **Enyi Majeshi ya Waislamu, kuubadilisha na kuwa sinagogi kwa wale waliofedheheshwa na kudhalilishwa!!**

**Enyi Waislamu:** Kadhia ya Palestina ni kadhia yenu, sio kadhia ya Shirika la Ukombozi, ambalo lilikuwa na bado lingali ni sehemu ya njama na zana ya kufilisi na kumaliza kadhia hii na kuitenganisha na kina chake cha Kiislamu na kuifanya iwe ya kadhia ya kitaifa. Ni kadhia ya wale wampendao Mwenyezi Mungu na Mtume wake, kwa hivyo harakisheni, **enyi Waislamu, simameni muinusuru Masra ya Nabii wenu, harakisheni kuyatakasa matukufu yenu**. Msikiti wa Al-Aqsa hautakombolewa kwa mazungumzo au kwa kutumia uhalali wa kimataifa au Baraza la Usalama, na hautalindwa na Jumuiya ya Nchi za Kiarabu, hizi ni taasisi za ulaji njama na usaliti. Badala yake, itakombolewa kama alivyoukomboa Salah ud-Din kwa jeshi lisiloshindika linalotamka Allahu Akbar (Mwenyezi Mungu ni Mkubwa zaidi), jeshi lenye wanaume wanaosonga mithili ya majabali na silaha zinazowahofisha maadui, **kwa hivyo pelekeni majeshi yenu kwa ajili ya kuinusuru Aqsa yenu.**

**Enyi Waislamu:** Msidanganyike na utawala na duru za Amerika, kwani ni dhaifu mno kuukabili Umma wa Uislam ikiwa utainuka kutokana na ukandamizaji wake na ukainuka kutoka usingizini mwake, na hautachelewesha ushindi wa Mwenyezi Mungu kwa waumini hata kwa saa moja. Ummah wa Uislamu sio kama China au Ufaransa, bali ni Umma wa vita vya muhimu kama vile Vita vya Qadisiyah, Yarmouk, Zallaqah, Mohacs, Ain Jalut na

***Endelea... UK 8***



Email: info@uqab.or.ke

Hittin. Inawezekana kwa Amerika kulitelekeza umbile la Kiyahudi kama ambavyo nchi za Ulaya zilivyo watelekeza Makruseda huko Jerusalem na kuwaacha wakabiliane na hatima yao isiyoweza kuepukika.

**Enyi Waislamu:** Palestina iko kwenye miadi na ukombozi, hivyo ni nani atakayepata heshima hii kubwa, kwa hivyo fanyeni bidii kuponya ugonjwa, kuondoa madhara ya maadui, na kuitakasa dunia yote iliyosalia kutokana na karaha ya wale waliomkasirisha Mwenyezi Mungu na Mtume wake, na kateni matawi ya ukafiri na kuung'oa. Siku zinahitaji kulipiza kisasi cha Kiislamu na wafuasi wa njia ya Muhammad, kusema mithili ya Jaji Mohieddin alivyosema katika hotuba ya ukombozi baada ya Salah ud-Din na Waislamu kuingia katika Msikiti wa Al-Aqsa.

**Enyi majeshi ya Waislamu, enyi Waislamu mulioko kila mahali, Msikiti wa Al-Aqsa unakuiteni na kutafuta nusra yenu, kwa hivyo je mtajibu wito huo?**

**Enyi Waislamu:** Jueni kwamba ahadi ya Mwenyezi Mungu hapana budi itatimia, Mwenyezi Mungu (swt) asema:

**وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ آمَنُوا مِنْكُمْ وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَيَسْتَخْلِفَنَّهُمْ فِي الْأَرْضِ كَمَا اسْتَخْلَفَ الَّذِينَ مِنْ قَبْلِهِمْ وَلَيُمَكِّنَنَّ لَهُمْ دِينَهُمُ الَّذِي ارْتَضَى لَهُمْ وَلَيُبَدِّلَنَّهُمْ مِنْ بَعْدِ خَوْفِهِمْ أَمْناً يَعْبُدُونَنِي لَا يُشْرِكُونَ بِي شَيْئاً وَمَنْ كَفَرَ بَعْدَ ذَلِكَ فَأُولَئِكَ هُمُ الْفَاسِقُونَ**

**“Mwenyezi Mungu amewaahidi wale walio amini miongoni mwenu na wakatenda mema, ya kwamba atawafanya makhalifa katika ardhi kama alivyo wafanya makhalifa wa kabla yao, na kwa yakini atawasimamishia Dini yao aliyo wapendelea, na atawabadilishia amani baada ya khofu yao. Wawe wananiabudu Mimi, wala wasinishirikishe na chochote. Na watao kufuru baada ya hayo, basi hao ndio wapotovu.”** [An-Noor: 55]. Mwenyezi Mungu (swt) asema:

**فَإِذَا جَاءَ وَعْدُ الْآخِرَةِ لِيَسُوءُوا وُجُوهَكُمْ وَلِيَدْخُلُوا الْمَسْجِدَ كَمَا دَخَلُوهُ أَوَّلَ مَرَّةٍ وَلِيُتَبِّرُوا مَا عَلَوْا تَتْبِيراً**

**“Na ikifika ahadi ya mwisho ili waziharibu nyuso zenu, na waingie Msikitini kama walivyo ingia mara ya kwanza, na waharibu kila walicho kiteka kwa uharibifu mkubwa”** [Al-Isra: 7].

Mtume (saw) amesema:

**لَا تَقُومُ السَّاعَةُ حَتَّى يُقَاتِلَ الْمُسْلِمُونَ الْيَهُودَ، فَيَقْتُلُهُمُ الْمُسْلِمُونَ حَتَّى يَخْتَبِئَ الْيَهُودِيُّ مِنْ وَرَاءِ الْحَجَرِ وَالشَّجَرِ، فَيَقُولُ الْحَجَرُ أَوِ الشَّجَرُ: يَا مُسْلِمُ يَا عَبْدَ اللَّهِ هَذَا يَهُودِيٌّ خَلْفِي، فَتَعَالَ فَاقْتُلْهُ، إِلَّا الْغَرْقَدَ، فَإِنَّهُ مِنْ شَجَرِ الْيَهُودِ**

**“Hakitasimama Kiyama mpaka Waislamu wapigane na Mayahudi; Waislamu watawauwa Mayahudi mpaka Yahudi atajificha nyuma ya jiwe na mti, kisha jiwe au mti huo utasema: Ewe Muislamu, ewe mja wa Mwenyezi Mungu huyu hapa Yahudi nyuma yangu, basi njoo umuuwe; isipokuwa mti wa Gharqad, kwani huo ni katika miti ya Mayahudi.”**

**Enyi Waislamu, songeeni mara moja, songeeni sasa kuinusuru Dini yenu na Al-Aqsa yenu, songeeni kupata heshima ya kusimamisha Dini na kuikomboa Ardhi Iliyobarikiwa, kwani nyinyi ni kizazi cha Salah ud-Din, kwa hivyo mleteni miongoni mwenu Salah mpya wa kuitakasa Al-Aqsa kutokana na najisi ya Mayahudi.**

Ee Mwenyezi Mungu, tunakuomba uturuzuku Khilafah Rashida kwa njia ya Utume, kuisimamisha Dini, kuwanusuru Waislamu, na kuikomboa Al-Aqsa iliyotekwa nyara.

**#Aqsa_calls_armies**

**#AqsaCallsArmies**

**#OrdularAksaya**

**#الأقصى_يستصرخ_الجيوش**





Email: info@uqab.or.ke

# Amerika Imekuwa Vipi Muathirika wa Hivi Karibuni Ndani ya Makaburi ya Himaya?

**Imeandikwa kwa Ajili ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir na**

**Adnan Khan**



Dunia inaendelea kuiangalia Afghanistan huku wengi bado wakishangaa vipi uvamizi wa miaka 20 umeshindwa kwa kiasi hicho cha kustaajabisha. Kiwango cha Raisi wa Amerika cha kukubalika kwa wananchi kimekuwa cha chini kabisa wakati watu wengi wakiangalia maamuzi ya kuboronga ya Amerika kwa kuwaondoa wafanya kazi wake na kuwaacha wale waliofanya kazi pamoja na Amerika. Mara tu baada ya kuondoka kwa Amerika mnamo Agosti 15, 2021 shirika lenye utata la serikali ya Amerika, Afisi Maalum ya Inspecta Mkuu kwa ajili ya Kuijenga Upya Afghanistan (Office of the Special Inspector General for Afghanistan Reconstruction), au SIGAR ilichapisha uchunguzi wake wa miaka 13 katika mafunzo ambayo yanahitaji kuchunguzwa katika uvamizi na ukaliaji wa Afghanistan. Shirika hili liliwahoji mamia ya washiriki katika vita ambapo ilikusudiwa kubaini kushindwa kwa sera nchini Afghanistan. SIGAR ilifanya mahojiano kwa zaidi ya miaka 13 na waundaji sera kadhaa, wanajeshi, wanasiasa na wengineo ambao walishiriki katika vita nchini Afghanistan. Ufahamu huu umefichua mwanga kwa uvamizi wa Amerika nchini Afghanistan na kwa nini ulishindwa.

Wengi kati ya waliohojiwa walikuwa wawazi katika tathmini yao kwani walitegemea kutofichuliwa wazi kauli zao. Nyaraka za SIGAR zinaonyesha kuwa Amerika haikutambua kabisa nini ilikuwa ikifanya Afghanistan. Je wanajeshi walikuwa kwa ajili ya kupambana na Al-Qaida au kuigeuza Afghanistan kuwa nchi ya kidemokrasia ya kisasa ya Kimagharibi? Inaelekea kana kwamba misheni haikuwa imeundwa, ikiruhusu siasa za Amerika kuburutwa kwa miongo, bila kuwa na lengo la wazi, mbinu zilibadilika vile vile. Vikosi vilisukumizwa nchini kisha vikatolewa. Dolari za Amerika zilienezwa katika uchumi wa Afghanistan, zikitengewa idadi isiyokwisha ya miradi bila kuwepo mpango mpana, ikihifadhi kila dolari iliotengwa na Bunge la Amerika.

Kuhusu vita vyenyewe, wale walioshiriki na wale waliowapeleka wanajeshi wa Amerika vitani kulikuwa na jitihada za wazi na endelevu kwa serikali ya Amerika kuudanganya umma kwa makusudi. Maafisa jijini Kabul – na katika ikulu ya White House – walikuwa wakiharibu takwimu ili ionekane kuwa Amerika ilikuwa ikishinda vita na hali ya kuwa hali haikuwa hivyo. Wote waliohojiwa kwa ajili ya ripoti ya mwisho walikubali kuwa hakukuwa na mkakati licha ya matamko yaliotolewa kwa umma.

Wengi bado wanajaribu kufahamu vipi jeshi la Afghanistan lililofunzwa na Amerika, likidhaminiwa kifedha na silaha lilijisalimisha kwa haraka mnamo Agosti 2021. Amerika imejaribu kuibua jeshi kutoka kwenye majivu nchini Afghanistan. Miaka baada ya miaka,

*Endelea... UK 10*

maafisa wa Amerika wameuhakikishia umma wa Amerika kuwa mpango ulikuwa ukifanya kazi na kuvipatia sifa vikosi vya Afghanistan. Lakini Amerika ilijaribu kuliunda jeshi kwa namna sawa na jeshi la Amerika, lenye kambi za kijeshi na miundo mbinu huku nchi ikiwa na miundo mbinu yake dhaifu, mwishowe jeshi lilibakia tu kwenye karatasi kwa kuwa wengi walihitaji kulipwa mishahara tu wakati uchumi ukianguka. Maafisa wengi pia waliunda wanajeshi hewa ili kujaza fedha mifukoni zilizotolewa na Amerika.

Barack Obama aliifanya Afghanistan kuwa ni kipaumbele chake kikuu katika kampeni yake. Aliamini kuwa Amerika imevipuuza vita halisi ilipovamia Iraq. Baada ya kufanya tathmini yake, aliamini kama mtangulizi wake kushinda vita na akamchagua David Petraeus na Generali Stanley McChrystal ili hatimaye kuibuka na ushindi nchini Afghanistan. Majenerali wote wawili walibuni mkakati wa kupambana na uasi ambao kwa kweli haukushughulikia suala husika. Mkakati wa kupambana na uasi ulikuwa ni sawa na uliojaribiwa mwaka 2004, lakini wakati huu ukiwa na kipote kidogo cha vikosi. Mpango wa McChrystal-Petraeus ulishindwa kutambua ima ni kupigana vita hasa Afghanistan, kushughulika na operesheni za amani, kuongoza mpango wa mafunzo, au kutekeleza kitu chengine. Licha ya kasoro hizi za wazi, Obama na serikali ya Amerika waliwaziba watu macho na kuutamkia umma kuwa mambo yalikuwa yanakwenda vizuri.

Wakati Donald Trump alipochukua uongozi wa ikulu ya White House licha ya mazungumzo yote juu ya mapigano, mkakati wake haukuwa tofauti na wa watangulizi wake na kitu pekee cha ziada kilikuwa ni uongo uliotumika kuhalalisha kubakia kwao nchini.

Ripoti ya SIGAR na msururu uliofuata wa (gazeti la) Washington Post wa nakala asili za zaidi ya kurasa 2,000 za mahojiano kwa watu 428 walioshiriki dori ya moja kwa moja katika vita unatoa uoni wa ndani kwenye vita vya Amerika nchini Afghanistan na orodha ya kushindwa pamoja na majigambo ya utekelezaji wa Amerika katika vita. Huku ripoti ya SIGAR ikiwa haiangazii kwenye malengo ya mikakati ya kwa nini Amerika imeivamia Afghanistan inatoa ufichuzi wa ufahamu wa namna Amerika imekuwa muathirika wa hivi sasa ndani ya makaburi ya Himaya (madola makuu).

# JIBU LA SWALI

# Ubebaji wa Da'wah ni Faradhi ya lazima ama ni Faradhi ya Kutoshelezana?



**Swali:**

Assalamu Alaykum Warahmatullahi Wabarakaatuhu

Mwenyezi Mungu akulipe kheri kwa niaba yetu na Mwenyezi Mungu aunusuru Uislamu na Waislamu kupitia mikono yako.

Swali langu ni, Je kubeba Daawah ni Faradhi ya lazima ama ni Faradhi ya kutoshelezana na je kubeba Daawah pamoja na kundi yachukua sifa ya kubeba daawah kama mtu binafsi.

Wabaaraka Llahu fiik

**Jibu:**

Waalaykum salam Warahmatullahi Wabarakaatuh

1- Kazi ya kusimamisha Khilafah ni Faradhi hadi itakaposimamishwa, Na kazi ya kurudisha maisha ya Kiislamu ni Faradhi mpaka yatakaporudishwa. Na kazi ya kurudisha Khilafah haiwezekani ila kwa kikundi "Kutla", Na Muislamu kuwapo katika kikundi kinachofanya kazi ya kurudisha maisha ya Kiislamu ni Faradhi, Lakini ni Faradhi ya kutoshelezana wala haipomoki kwa mwenye kukalifishwa na sheria (mukallaf) mwenye uweza mpaka yatakaporudishwa maisha ya Kiislamu kwa kusimamishwa Khilafah.

2- Ama kwanini ni Faradhi, ni kwa kauli yake Subhanahu:

وَلْتَكُن مِّنكُمْ أُمَّةٌ يَدْعُونَ إِلَى ٱلْخَيْرِ وَيَأْمُرُونَ بِٱلْمَعْرُوفِ وَيَنْهَوْنَ عَنِ ٱلْمُنكَرِ ۚ وَأُو۟لَٰٓئِكَ هُمُ ٱلْمُفْلِحُونَ

**"Na uwe kutokana na nyinyi umma unao lingania kheri na unao amrisha mema na unakataza maovu. Na hao ndio walio fanikiwa."** [Aali-Imran: 104]

Imekuja katika kitabu cha Utambulisho (Al Taarif) kuhusu tafsiri ya aya hii:

[... Mwenyezi Mungu ameawaamrisha Waislamu katika aya hii liwe miongoni mwao kundi lenye muundo, linalosimama mambo mawili:

**La kwanza:** Kulingania katika kheri,yaani Daawah kwa Uislamu.

**Na pili:** Kuamrisha mema, na kukataza muovu.

*Endelea... UK 12*


Email: info@uqab.or.ke

Na hii amri ya kusimamisha kundi lenye muundo ni mujarad wa ombi (Talab), lakini kumepatikana kiunganishi (Qarina) kinachotambulisha kuwa ni Amri ya lazima (Twalab Jaazim), kwani kazi ambayo imebainishwa na aya ili lisimame nayo hili kundi lenye muundo - kuanzia kulingania Uislamu, kuamrisha mema na kukataza maovu - ni jambo la Faradhi kwa Waislamu wasimame nalo, kama vile ambavyo imethibiti katika aya nyingi na hadith zinazotambulisha hayo, Amesema Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw):

وَالَّذِي نَفْسِي بِيَدِه لَتَأْمُرُنَّ بِالْمَعْرُوفِ وَلَتَنْهَوُنَّ عَنِ الْمُنْكَرِ أو لَيُوشِكَنَّ اللَّهُ أَنْ يَبْعَثَ عَلَيْكُمْ عِقَاباً من عِنْده ثُمَّ لَتَدْعُنَّهُ فَلاَ يَسْتَجِيبُ لَكُمْ

"**Na apa na yule ambaye nafsi yangu imo mikononi mwake mtaamrisha mema na mtakataza maovu au hivi karibuni Mwenyezi Mungu atawateremshia adhabu kutoka kwake kisha mtamuomba na hatowakubalia**" [Amepokea Ahmad] Kwa hiyo itakuwa hicho kiunganishi (Qarina) cha ombi (Twalab) ni cha lazima (Jazim) na amri kwayo itakuwa ni ya wajibu...] Mwisho.

3- Ama kwa nini ni Faradhi ya kutoshelezana, ni kwa kuwa aya ina maandishi ya neno ((منكم (Miongoni mwenu) basi hapo Faradhi katika hali hiyo ni ya kutoshelezana yaani kundi lenye muundo miongoni mwenu linalolingania kwa Uislamu (Wanalingania katika kheri). Na imekuja kwa maarifa kwa "Alif" na "Lam" kwa hiyo ni kwa ujumla yaani kwa Uislamu wote, na la juu zaidi Dola yake..

4- Ama uhalisia wa Faradhi ya kutoshelezana…

A- Imekuja katika Shakhsiya ya Kiislamu Juzuu ya Tatu mlango wa Wajib:

[Ama Faradhi kwa upande wa kusimama nayo ni vigawanyo viwili: Faradhi ya lazima, na Faradhi ya kutoshelezana, na hakuna tofauti kati yake katika uwajibu; Kwa kuwa uwajibu ni mmoja kwazo, nayo ni kwa kuwa Faradhi ya lazima imetakwa ifanywe na kila mmoja mwenyewe, Na Faradhi ya kutoshelezana imetakwa ifanywe na Waislamu wote, Ikiwa imefikiwa kutoshelezana kwa kusimamisha basi Faradhi imepatikana, Sawa iwe amesimamisha kila mmoja miongoni mwao, au wakasimama nayo baadhi yao, na isipofikiwa kutoshelezana kwa kusimama nayo basi Faradhi inaendelea kusimama kwa kila mmoja miongoni mwao mpaka ifanywe ile faradhi].

B- Na imekuja katika Shakhsiya ya Kiislamu Juzuu ya Pili:

(Kwamba kumsimamisha Khalifah ili asimamishe Hukmu za Uislamu na kubeba Daawah yake ni Faradhi kwa Waislamu na ni jambo lisilo na tashwishi (shubha) katika kuthubutu kwake katika nususi za kisheria sahihi, juu ya kuwa ni Faradhi kwa upande unaolazimishwa na Faradhi ambayo Uislamu umefaradhisha juu ya Waislamu kusimamisha hukmu ya Uislamu na kulinda yai la Waislamu, Isipokua hii Faradhi ni Faradhi ya kutoshelezana, wakisimamisha baadhi Faradhi imepatikana na kupomoka kwa waliobakia, na ikiwa baadhi hawakuweza kuisimamisha na hata kama wamesimama na kazi za kuisimamisha basi itabakia kuwa ni Faradhi kwa Waislamu wote, Na wala haipomoki Faradhi kwa Muislamu madam Waislamu hawana Khalifa.)

C- Na imekuja katika kitabu cha Fikra ya Kiislamu:

(.. Faradhi ni hotuba ya Al shaari' inayoambatana na kutaka kufanywa kitendo matakwa ya lazima, kama kauli yake taa'la

أَقِيمُوا الصَّلاةَ

**"Na shikeni Swala"** [Al-Baqara: 43].

انْفِرُواْ خِفَافًا وَثِقَالاً وَجَاهِدُواْ بِأَمْوَالِكُمْ وَأَنفُسِكُمْ فِي سَبِيلِ اللهِ

**"Nendeni mtoke, mkiwa wepesi na wazito, na piganeni Jihadi kwa mali yenu na nafsi zenu katika Njia ya Mwenyezi Mungu."** [At-Tawba: 41].

Na kama kauli yake (saw):

إِنَّمَا جُعِلَ الإِمَامُ لِيُؤْتَمَّ بِهِ

**"Hakika amewekwa imamu ili watu wamfuate - watimize Swala wakiwa nyuma yake"**

مَنْ مَاتَ وَلَيْسَ فِي عُنُقِهِ بَيْعَةٌ مَاتَ مِيتَةً جَاهِلِيَّة

**"Atakayekufa na katika shingo yake hana ahadi ya utiifu (Ba'yah) amekufa kifo cha kijahilia".**

Hizi nususi zote ni hotuba kutoka kwa Al Shaari' inayoambatana na ombi la lazima la kufanywa kitendo. Na kiunganishi (Qarina), ndio inayolifanya ombi kuwa la lazima ambayo imekuja kuhusiana na ombi hilo (talab) na ikalifanya kuwa la lazima (jazim), hivyo ni wajib kutekelezwa...

Na juu ya hayo ni makosa kusema kuwa Faradhi ya kutoshelezana ni ile ambayo wakisimama nayo baadhi inapomoka kwa waliobakia, Bali Faradhi ya kutoshelezana (Fardhu Kifaya) ni ile ambayo wakiisimamisha baadhi hupomoka kwa waliobakia. Na kupomoka kwake wakati huo ni jambo la kiuhalisia, kwani kitendo kilichotakiwa kufanywa kimesimama, na kikapatikana, Na hakuna nafasi ya kubakia kitendo hicho, Hii ndio Faradhi ya kutoshelezana, nayo ni kama Faradhi ya lazima (Fardhu A'in) sawa kwa sawa...)

Nataraji iwe haya yanatosheleza na Allah anajua zaidi na ni mwenye hikma zaidi.

**Ndugu Yenu**

**Ata Bin Khalil Abu Rashtah**



Email: info@uqab.or.ke